

## **Kanisa lisimwache hata mtu mmoja nyuma**

Na Mchg. Dkt. Martin Junge

Bwana Yesu alipokuwa akitoa huduma aliwaendea watu jinsi walivyokuwa na kuwafuata pale walipokuwa wakiishi – aliwafuata wakiwa na dini zao na katika maeneo yao. Aliwatambua alipokutana nao na hakumwacha hata mmoja nyuma.

Kwa sababu hiyo, wapo waliohoji ni kwa nini anakula na wenye dhambi na kuwatembelea. Kanisa leo linaitwa lisiache hata ‘kondoo mmoja nyuma’. Somo ni kutoka Luka 15: 2-7 linalohusu habari ya ‘kondoo aliyepotea’.

Kanisa linapewa wito kwamba lisimwache hata mtu mmoja nyuma; bali limtafute mtu huyo kama kondoo mmoja aliyepotea kati ya kondoo 100. Katika somo hili tunaona mchungaji aliwaacha wale 99 kondoo nyikani na kwenda kumtafuta yule mmoja aliyepotea na kumrudisha kundini.

Yesu alipokuja duniani alidhihirisha kwamba Yeye ni Mungu kweli na binadamu kweli. Na katika kueneza Neno alitumia mifano iliyokuwa rahisi kueleweka katika jamii aliyoihudumia. Tunaona katika mfano huu (Luka 15: 2-7): Jambo la kwanza kuna kundi lililotawanyika na kondoo mmoja kabaki nyuma. Pili ni kama vile Yesu anatumkumbusha kuhusu wagonjwa katika jamii yetu; na watu waliovunjika moyo na jamii isiyo na umoja.

Mwisho mfano huu unaeleza kuhusu mwana mpotevu ambapo kuna ambao hawakufurahi alipopokelewa kwa shangwe baada ya kurudi nyumbani kwa baba yake. Hii inatufundisha kwamba hata wale ambao hawafurahii kitendo cha aliyepotea kurudi kundini na wao pia wamepotea.

Changamoto ya leo ni kwa watu kutengwa kwa kutotendewa haki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Tunashuhudia kuongezeka kwa ufa kati ya matajiri na maskini na machafuko ambapo kanisa katika mahali tulipo na kimataifa; linapaswa kuchukua hatua na kutoa kauli kuhusu uonevu kama huo. Kutenga ni dalili za kukosa uadilifu.

Umoja wenu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na namna yenu ya kutatua tofauti miongoni mwenu; ni kipawa chema kwa watu wenu. Mnavyotembea, kushuhudia na kuhudumia jamii kwa pamoja ni mambo muhimu yanayofahamika hadi nje ya mipaka ya kanisa.

Kiini cha ujumbe huu ni kwamba Mungu ni mwingi wa rehema, huruma tele na haki; sifa ambazo wanadamu hatuna. Neema ya Mungu kumkomboa mwanadamu haitokani na uwezo tulionao bali inatokana na asili ya Mungu alivyo. Hivyo tuige mafundisho yake Yesu kwa kuhakikisha hakuna atakayepotea na hatumbakizi hata mtu mmoja nyuma. Tuache mtazamo wa kuwabagua wenzetu; tuwakaribishe kama Kanisa kwa kutoa huduma za kijamii kwa mfano kuwasaidia wanaohitaji chakula, nk.

KKKT kwa kupitia Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Tanzania (TCRS), linanalo hisaniwa na FMKD, linahudumia maelfu ya wakimbizi kutoka Burundi. Pongezi KKKT kwa kutoa huduma hiyo kwa niaba ya makanisa 145 ya FMKD.

Mfano huu uigwe na Kanisa kwa ujumla popote lilipo kwa kuendelea kutangaza Injili na kutoa huduma za kijamii na udikonia kwa watu wanaoteseka katika jamii na katika makanisa. Hii ni kuishi kwa vitendo wito wa kutoacha wengine bali kuwakubali na kuwashirikisha.

Tunashukuru Kanisa kwa kampeni ya kupanda miti ili kuhifadhi mazingira. Askofu Dkt. Fredrick Shoo anafahamika kama “Askofu wa Miti” kwa kujitoa kwake katika kampeni ya upandaji miti. Kati ya mwaka 1997 na 2016 Dayosisi imepanda miti 1,978,112 na lengo ni kufika miti 3,237,400 ifikapo 2020.

Kanisa linahitaji kutoa sauti yake ya unabii kujenga umoja na kuingilia kati pale haki inapokosekana na kusababisha faraka na kubaguliwa na jamii badala ya kuwajengea watu matumaini.

Watu wanahitaji kuona alama ya matumaini wakitazama milima kupata matumanini na kutiwa moyo na kuachana na magomvi pia kwa kukubali kutofautiana kwa njia ya amani.

(Mchg. Dkt. Junge ni Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) ambaye alitoa mahubiri haya akiwa Tanzania).